**(IJA)**
**CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA**
**LUSHOTO**

# MAELEZO YA MKUU WA CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA LUSHOTO KATIKA MAHAFALI YA 19 YA CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA LUSHOTO TAREHE 29 NOVEMBA, 2019 YALIYOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA NYALALI, IJA - LUSHOTO

Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Profesa Ibrahim Juma, (PhD),

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Mheshimiwa Dkt. Gerald Ndika, Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania;

Waheshimiwa Majaji Wafawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Tanga na Moshi;

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,

Wajumbe wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto;

Viongozi Waandamizi wa Chuo,

Viongozi mbalimbali wa Serikali;

Wahadhiri na Watumishi wote wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto;

Wazazi, Walezi, Ndugu na Marafiki wa Wahitimu wetu;

Wageni Waalikwa;

Wahitimu wote waliosoma IJA ambao wamehudhuria Mahafali ya leo;

Wapendwa Wahitimu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto,

Mabibi na Mabwana,

Habari za Asubuhi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa vyote vilivyopo kwenye ardhi hii kwa kututunuku uhai na siha njema iliyotufanya sio tu kufurahia vilivyopo kwenye ardhi yake bali pia kutuwezesha kujumuika sote kwa pamoja katika sherehe ya mahafali ya 19 ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Aidha, ninayo furaha na heshima kubwa kukukaribisha wewe binafsi pamoja na hadhara hii kubwa katika mahafali haya. **Karibuni sana.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**, mimi binafsi, Menejimenti na wanajumuiya wote wa Chuo tumejaa bashasha kwa ujio wako na kwa heshima kubwa tukushukuru sana kwa kukubali mwaliko wetu kuja kushiriki pamoja nasi katika sherehe za mahafali ya 19 ya Chuo. Tunatambua kwamba, mbali na majukumu yako mengi ya kitaifa na kifamilia umeweka kipaumbele cha kujumuika nasi kwenye shughuli hii kubwa kwenye kalenda ya shughuli za Chuo.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** naomba kukufahamisha wewe pamoja na hadhara hii kuwa leo hii jumla ya wahitimu **403** watatunukiwa Stashahada na Astashahada ya Sheria. Kati ya hao wahitimu wa Stashahada ya Sheria ni **169** na wa Astashahada ya Sheria ni **234** hivyo kufanya idadi ya wahitimu waliomaliza hapa chuoni tangu kuanzishwa kwake kufikia **6037.** Katika takwimu hizi za wahitimu wa leo, kwa upande wa Stashahada ya Sheria kati ya wahitimu **169** wanaume ni **93 (55.03%)** na wanawake **76 (44.97%)** na kwa

upande wa Astashahada ya Sheria, kati ya wahitimu **234** wanaume ni **102 (43.59%)** na wanawake ni **132 (56.41%)**.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** napenda pia kuchukua fursa hii kutoa taarifa kwamba, wahitimu wanaotunukiwa vyeti vyao leo walianza mafunzo yao katika mwaka wa masomo 2017/18 kwa kozi ya Stashahada ya Sheria ambayo ni ya miaka miwili. Kwa upande wa kozi ya Astashahada ya Sheria ambayo ni ya mwaka mmoja walianza mafunzo katika mwaka wa masomo 2018/19.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** napenda pia kukufahamisha kwamba, katika mwaka wa masomo 2019/20 Chuo kimedahili jumla ya wanachuo wapya **675** kwa mchanganuo ufuatao; **317** wanachuo kwa kozi ya Stashahada ya Sheria na wanachuo **358** kwa kozi ya Astashahada ya Sheria.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** naomba nitoe mwelekeo wa Udahili kitakwimu kwa takribani miaka mitatu mfululizo kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na. 1: Mwelekeo wa Udahili Miaka mitatu Mfululizo 2017/2018-2019/2020**

| MWAKA WA MASOMO | WALIODAHILIWA KOZI YA STASHAHADA YA SHERIA | WALIODAHILIWA KOZI YA ASTASHAHADA YA SHERIA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 2017/2018 | 249 | 289 | 538 |
| 2018/2019 | 290 | 367 | 657 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2019/2020 | 317 | 358 | 675 |
| **JUMLA** | **856** | **1,014** | **1,870** |

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo juu, kumekuwa na ongezeko la kila mwaka la udahili na kwa mwaka wa masomo 2017/18 ongezeko lilikuwa asilimia 29 ukilinganisha na mwaka wa masomo 2016/17 na kwa mwaka wa masomo 2019/20 kumekuwa na ongezeko la asilimia 2.7 Ukilinganisha na mwaka wa masomo 2018/19. Mwenendo huu wa udahili ambao unaonesha ongezeko la kila mwaka umechangiwa na juhudi zinazofanywa na watumishi pamoja na Menejimenti ya Chuo katika kukitangaza Chuo sehemu mbalimbali katika matukio ya Sikukuu za Kitaifa na kupitia vyombo vya habari sambamba na kutoa elimu na huduma bora kwa wanachuo wetu. Aidha, wahitimu wetu pamoja na wanachuo nao wamekuwa mabalozi wetu wakubwa katika kukitangaza Chuo kwa ndugu, jamaa, marafiki na jamii inayowazunguka.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** katika kutimiza dira na dhima ya chuo, siku zote tumekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza mpango mkakati ambao tumejiwekea. Muda hauniruhusu kuzungumzia vipengele vyote vya Mpango mkakati wa chuo na utekelezaji wake kwa undani. Niseme tu kwa kifupi kwamba utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Chuo wa Miaka mitano wa mwaka 2018/19 mpaka mwaka 2022/23 unaendelea kutekelezwa ipasavyo. Naomba niruhusu nitaje baadhi ya mikakati ambayo

Chuo kimejiwekea na kinatekeleza katika Mpango Mkakati kwa sasa katika kufanikisha azma ya kuanzishwa kwake.

1. Chuo kimeendelea kutoa Mafunzo Endelevu ya Kimahakama pamoja na Mafunzo Elekezi kwa Majaji wa Mahakama Kuu na Rufani pamoja na watumishi wengine wa Mahakama wakiwemo Mahakimu wenye mamlaka ya ziada yaani *Extended Jurisdictions*.

2. Chuo kimeendelea kufanya Tafiti na Ushauri kwa Mahakama ya Tanzania na wadau wengine wa maendeleo ikiwemo utafiti kuhusu hali halisi ya mahakama za watoto na uendeshaji wa mashauri kwenye mahakama hizo, tathmini ya mafunzo yanayotolewa kwa wadau wanaohusika na mashauri ya mtoto na utafiti kuhusu uwezo wa utendaji kazi wa Mabaraza ya Kata. Tafiti hizi zinasaidia kutatua changamoto za kiutendaji sio tu kwa watawala wa Mahakama bali pia kwa maafisa watendaji ambao wanahusika mojakwamoja na utekelezaji wa sharia hiyo.

3. Vilevile Chuo kimeendelea kutoa mafunzo kwa wadau wote wanaoshughulika na mashauri ya kesi za watoto yaani "*Juvenile Justice Frontline Workers*" wakiwemo Mahakimu, Mawakili wa Serkali, Waendesha Mashtaka, Maafisa Ustawi wa Jamii na Mawakili wa Kujitegemea mafunzo ambayo yameendeshwa kwenye kanda zote za Mahakama Kuu ya Tanzania isipokuwa Songea na Mtwara ambazo tunarajia kufikia mwezi wa pili mwakani tutakuwa tumezifikia. Jumla ya wadau 593 wamekwisha pata mafunzo hayo ambayo

kutokana na tathmini tuliyofanya tumegundua yameboresha sana utoaji haki kwa sio tu kwa mtoto lakini pia kwa kina mama katika eneo la matunzo kwa watoto pamoja na kutambua vinasaba vya watoto hao kisheria (*Parentage*).

4. Chuo kimeendelea kutoa machapisho mbali mbali kwa matumizi ya Mahakama ya Tanzania ikiwemo *Bench Books* kwa ajili ya Majaji, *Quick Reference* kwa ajili ya Mahakimu wa Mahakama za Wilaya na Mahakimu Wakazi, *Handbook* kwa jili ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, pamoja na *Manual* ya Kuwaandaa Naibu Wasajili, Mahakimu Wafawidhi vile vile *Manual* za kufundishia Madalali na Wasambaza Nyaraka wa Mahakama.

5. Sambamba na hilo Chuo kimeingia makubaliano na Shiriki la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO). Makubaliano hayo yamekiwezesha Chuo kuandaa muongozo wa kufundishia (*Training Manual*), ambao umetolewa maoni na wadau mbalimbali wakiwemo Mahakama ya Tanzania, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Tume ya Kurekebisha Sheria, Ofis ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mawakili wa Kujitegemea. Sambamba na hilo, Chuo pia kimeandaa Mtaala wa kufundishia pamoja na kutoa mafunzo kwa watendaji wa mabaraza ya ardhi ya vijiji na kata pamoja na kuwaalika maafisa wa wilaya wanaoshughulikia migogoro ya ardhi. Mafunzo hayo kwa kuanzia yamefanyika katika wilaya za

Mvomero na Kilosa ambapo jumla ya washiriki **100** wamenufaika na mafunzo.

6. Aidha katika mwaka wa fedha 2019/20 chuo kupitia kitengo chake cha msaada wa kisheria yaani *IJA Legal Aid Unit* kwa kushirikiana na wahitimu wa IJA pamoja na Chama cha Wanasheria Tanganyika *(TLS)* kimetoa huduma ya Msaada wa Kisheria kwa wananchi wa maeneo ya Lushoto, Mlalo na Korogwe. Hii ni katika kufanikisha jitihada zetu za kuwafikia wale wote wenye uhitaji wa msaada wa kisheria wakiwemo wajane, wazee na watoto na hivo kuleta manufaa kwa jamii inayotuzunguka.

7. Chuo katika kukuza hadhi yake kama taasisi ya elimu ya juu kimeendelea kutoa machapisho mbali mbali ikiwemo jarida la kitaaluma la *IJA Journal* ambalo limevutia wachapishaji wa ndani na nje ya chuo. Jarida hilo linaongozwa na Bodi ya ushauri inayoundwa na wanataaluma wabobezi ikiwemo majaji kutoka nchi mbali mbali za Afrika.

8. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo kwa Madalali na Wasambaza Nyaraka wa Mahakama kwa zaidi ya mwaka sasa ambapo jumla ya washiriki 98 wamepatiwa mafunzo hayo.

9. Chuo kimeendelea kupanua wigo wa kutoa mafunzo endelevu kwa wadau mbalimbali wa Tanzania Visiwani ikiwemo wajumbe wa Bodi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Zanzibar pamoja na majaji na mahakimu Mahakama ya Zanzibar.

10. Chuo kimeendelea kuunda mifumo ya kiteknolojia na kuzidisha matumizi ya TEHAMA katika kufundishia, utawala pamoja na kuendesha mafunzo ya kimahakama.

11. Chuo kimeendelea kuboresha miundo mbinu pamoja na huduma za kijamii. Nichukue fursa hii kuwashukuru wenzetu wa Mamlaka ya Maji vijijini kwa kututatulia chamgamoto ya upatikanaji wa maji ambayo tuliihesabu ni kero sugu kwa miaka mingi hapa chuoni.

12. Chuo kimezidi kusimamia suala la nidhamu kwa wanachuo na watumishi kupitia Kamati mbali mbali ikiwemo Kamati ya Maadili.

13. Chuo kimezidi kusimamia ubora pamoja na usimamizi wa rasilimali kupitia kamati mbali mbali na hii imedhihirishwa na kupata hati safi kila mwaka, kupata Ithibati ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE),* kupata hati ya usalama wa mtandao yaani *Vulnerability Test* kutoka Mamlaka ya Mawasilinao Nchini *(TCRA).*

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** baada ya kuelezea machache kuhusu utekelezaji wa mpango mkakati, naomba sasa kuchukua fursa hii kuwapongeza wahitimu wote watakaotunukiwa Astashahada na Stashahada ya Sheria ya Sheria ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. **Hongereni sana**. Niwaombe wahitimu wetu wa leo waenzi juhudi zilizooneshwa na wale wote waliohusika katika mchakato wenu wa kupata elimu na hatimaye kufanikisha uhitimu wenu siku ya leo. Kwa kufanya hivyo mtatoa mchango mkubwa

kwa taifa na hivyo kuwa faraja kubwa kwa wazazi na walezi waliojitoa kwa hali na mali kuwasaidia katika masomo yenu. Kwetu sisi kama Chuo hii ni fahari kubwa kwa jamii inayotuzunguka na Taifa kwa ujumla.

Ni matumaini yangu kuwa wahitimu wote mtaendelea kuwa mabalozi wetu wazuri katika jamii kwa kuwa raia wema wenye tabia njema na mahusiano mema katika maeneo yenu ya kazi na vyuoni kwa wale watakaoendelea na masomo kama ambavyo wamefanya wenzenu waliowatangulia kuhitimu katika Chuo hiki.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** baada ya kusema hayo, naomba sasa kwa heshima nimkaribishe Mheshimiwa Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji Dkt Gerald Ndika, Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo ili aweze kutoa hotuba yake na hatimaye kukukaribisha wewe mgeni rasmi kuongea na wahitimu wote waliohudhuria.

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza na nawatakia wote kila la kheri katika kukamilisha mahafali na safari ya kurudi katika sehemu zetu za makazi na kazini.**

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu kibariki Chuo chetu cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na wanajumuiya wote.

**IJUMAA, 29 NOVEMBA 2019**